**SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALI MBALI
NA KUWEKA MASHARTI BORA NDANI YAKE**

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU


**VIFUNGU** **MAELEZO**

**SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI**

1. Jina fupi na kuanza kutumika.

2. Marekebisho ya Sheria mbali mbali.

**SEHEMU YA PILI
MAREKEBISHO YA SHERIA YA AFISI YA MWANASHERIA MKUU
(UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU), NAM. 6 YA 2013**

3. Kusomwa.

4. Marekebisho ya kifungu cha 3.

5. Marekebisho ya kifungu cha 14.

6. Kuongeza vifungu vipya vya 23A na 23B.

7. Kuongeza kifungu kipya cha 31A.

**SEHEMU YA TATU
MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA
NA DAWA ZA KULEVYA, NAM. 8 YA 2021**

8. Kusomwa.

9. Marekebisho ya kifungu cha 2.

10. Marekebisho ya kifungu cha 16.

11. Marekebisho ya kifungu cha 19.

12. Marekebisho ya kifungu cha 21.

13. Marekebisho ya kifungu cha 22.

14. Marekebisho ya kifungu cha 23.

15. Marekebisho ya kifungu cha 30.

16. Marekebisho ya kifungu cha 37.

17. Kuongeza kifungu kipya cha 41A.

18. Marekebisho ya kifungu cha 42.

19. Marekebisho ya kifungu cha 43.

20. Marekebisho ya kifungu cha 46.

21. Marekebisho ya kifungu cha 48.

22. Marekebisho ya kifungu cha 50.

23. Marekebisho ya kifungu cha 61.

24. Kufuta na kuweka badala yake kifungu kipya cha 72.

25. Kuongeza kifungu kipya cha 76A.

26. Marekebisho ya Jadweli la Tano.

**SEHEMU YA NNE**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA SHIRIKA LA MAWASILIANO ZANZIBAR, NAM. 4 YA 2023**

27. Kusomwa.

28. Marekebisho ya kifungu cha 3.

**SEHEMU YA TANO**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO, NAM. 1 YA 2003**

29. Kusomwa.

30. Marekebisho ya kifungu cha 4.

## SEHEMU YA SITA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA KIKOSI CHA VALANTIA, NAM. 5 YA 2004

31. Kusomwa.

32. Marekebisho ya kifungu cha 4.

33. Marekebisho cha kifungu cha 25.

## SEHEMU YA SABA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA WAKALA WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI ZANZIBAR, NAM. 2 YA 2022

34. Kusomwa.

35. Marekebisho ya kifungu cha 2.

36. Marekebisho cha kifungu cha 6.

37. Marekebisho ya kifungu cha 42.

**SHERIA NAM. 5 YA 2024**

**NIMESAINI**

**{DKT. HUSSEIN ALI MWINYI}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

..........05/07/.........., **2024**

# SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALI MBALI NA KUWEKA MASHARTI BORA NDANI YAKE

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali, 2024 na itaanza kutumika mara baada ya kutiwa saini na Rais.

Marekebisho ya Sheria mbali mbali.

**2.** Sheria zilizotajwa katika sehemu mbali mbali za Sheria hii zinarekebishwa kwa namna zilivyoainishwa katika sehemu husika.

## SEHEMU YA PILI
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA AFISI YA MWANASHERIA MKUU (UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU), NAM. 6 YA 2013

Kusomwa.

**3.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu (Utekelezaji wa Majukumu), Nam. 6 ya 2013 ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 3.

**4.** Kifungu cha 3 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika ufafanuzi wa neno "huduma za kisheria" kwa kuingiza maneno "mapitio ya sheria" baina ya maneno "uandishi wa sheria" na "na nyengine".

Marekebisho ya kifungu cha 14.

**5.** Kifungu cha 14 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (1) kwa:

(a) kuingiza aya mpya **za** (m), (n), (o), (p), (q) na (r) mara baada ya aya (l) kama ifuatavyo:

"(m) kuchukua na kufanya mapitio ya sheria za Zanzibar kwa lengo la kuziendeleza na kurekebisha mifumo yake;

(n) kuzifanya sheria za Zanzibar katika lugha nyepesi;

(o) kuandaa na kuwasilisha kwa Serikali programu ya uchunguzi wa sheria mbalimbali kwa lengo la kuzibadilisha sheria hizo kila baada ya muda, ikijumuisha mapendekezo;

(p) kuanzisha mfumo kwa ajili ya kupata taarifa yoyote inayohusiana na mifumo ya sheria ya nchi nyengine ambayo inaweza kuwezesha utekelezaji wa kazi zake;

(q) kuchapisha au kuwezesha uchapishaji wa mambo yanayohusiana na sheria au mambo mengine yanayohusika; na

(r) kuitisha, kuwezesha au kushajihisha uandaji wa semina, mafunzo, mihadhara na mikutano mengine ya umma kwa madhumuni ya usambazaji wa taarifa au mambo yanayohusiana na mabadiliko ya sheria kwa Zanzibar."

(b) kuzipa nambari upya aya zilizobaki kwa mpangilio wake.

Kuongeza vifungu vipya vya 23A na 23B.

**6.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza vifungu vipya vya 23A na 23B mara baada ya kifungu cha 23 kama ifuatavyo:

"Afisi kuushirikisha umma katika kufanya mapitio ya sheria.

**23A.**-(1) Afisi inaweza, katika kufanya uchunguzi wa jambo lolote, kupanga kazi zake kwa lengo la kuiwezesha kutoa elimu kwa umma juu ya masuala yanayohusiana na jambo hilo na kupata maoni ya idadi kubwa ya wananchi wa Zanzibar katika masuala husika.

(2) Kwa madhumuni ya kuendana na masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Afisi inaweza kufanya jambo lolote ambalo ni muhimu ili kufanikisha ushiriki wa umma katika kazi za Afisi na inaweza:

(a) kuandaa na kufanya semina kwa ajili ya majadiliano ya masuala ya umma yanayohusiana na jambo linalokusudiwa;

(b) kupanga mafunzo yatakayotolewa na Afisi kwa ajili ya umma;

(c) kuitisha na kushajihisha mijadala ya wazi kupitia Afisi au vyombo vya habari;

(d) kuanzisha na kuchapisha jarida au machapisho mengine kwa madhumuni ya kusambaza taarifa juu ya mabadiliko ya sheria; na

(e) kufanya jambo lolote ambalo ni muhimu kwa madhumuni ya kutangaza mapendekezo ya mabadiliko ya sheria na kupata uelewa wa wananchi na majibu yao.

Mambo ya kuzingatia wakati wa mapitio ya sheria.

**23B.-**(1) Afisi itazingatia mahitaji ya kuwa na sheria ambazo zipo kwa mujibu wa sera na mikakati ya kitaifa.

(2) Afisi itazingatia na kutoa mapendekezo kwa ajili ya mabadiliko ya sheria kwa lengo la kuhakikisha kuwa sheria za Zanzibar zinatungwa kwa ajili ya:

(a) kukuza na kuongeza wigo wa misingi mikuu ya haki za binadamu kama ilivyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 na Katiba ya Zanzibar ya 1984;

(b) kukuza na kulinda mila, maadili na imani za watu wa Zanzibar ambazo zinafaa kutumika kulingana na maendeleo ya kisasa ya mawazo ya kisheria;

(c) kukuza na kuhakikisha heshima ya utawala wa sheria;

(d) kuhakikisha maendeleo ya mfumo wa haki kwa ajili ya utoaji haki sawa na ulinzi bora wa mali ya jamii na mtu binafsi ya watu wa Zanzibar; na

(e) kukuza na kuimarisha heshima kwa haki za binadamu na watu wote katika mwenendo wao au biashara rasmi na masuala binafsi."

Kuongeza kifungu kipya cha 31A.

**7.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 31A mara baada ya kifungu cha 31 kama ifuatavyo:

"Kufuta na kubakiza.

**31A.**-(1) Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar, Nam. 16 ya 1986 inafutwa.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki;

(a) jambo lolote ambalo halijakamilika chini ya Sheria iliyofutwa litaendelea na kukamilishwa chini ya masharti ya Sheria hii; na

(b) wafanyakazi, mali na madeni chini ya Sheria iliyofutwa, yanahamishiwa kwa Afisi."

## SEHEMU YA TATU
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA ZANZIBAR, NAM. 8 YA 2021

Kusomwa.

**8.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar, Nam. 8 ya 2021 ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 2.

**9.** Kifungu cha 2 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta aya ya (a) katika ufafanuzi wa neno "Mahakama yenye uwezo" na kuweka badala yake aya mpya ya (a) kama ifuatavyo:

"(a) kuhusiana na makosa chini ya vifungu vya 21, 22, 30 na 38 ni Mahakama Kuu."

Marekebisho ya kifungu cha 16.

**10.** Kifungu cha 16 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongeza maneno "au faini inayolipwa kutokana na adhabu iliyotolewa na Mahakama" baina ya maneno "iliyofilisiwa" na "chini" katika kifungu kidogo cha (2)(c).

Marekebisho ya kifungu cha 19.

**11.** Kifungu cha 19 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongeza maneno "na katika mazingira yoyote kifungo kisichopungua miaka thelathini" mwishoni mwa kifungu.

Marekebisho ya kifungu cha 21.

**12.** Kifungu cha 21 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (1) kwa kuongeza maneno "na katika mazingira yoyote kifungo kisichopungua miaka thelathini," mwishoni mwa kifungu kidogo.

Marekebisho ya kifungu cha 22.

**13.** Kifungu cha 22 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (1) kwa kuongeza maneno "na katika mazingira yoyote kifungo kisichopungua miaka thelathini" mwishoni mwa kifungu kidogo.

Marekebisho ya kifungu cha 23.

**14.** Kifungu 23 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kufuta kifungu kidogo cha (1) na kuweka badala yake kifungu kidogo kipya cha (1) kama ifuatavyo:

"(1) Mtu ambaye atakuwa na kiwango kidogo cha aina yoyote za dawa za kulevya ambacho hakijaidhinishwa na daktari kwa ajili ya sababu za kimatibabu, ametenda kosa na akitiwa hatiani, ikiwa dawa za kulevya zinazohusishwa:

(a) ni zile zilizotajwa chini ya Sheria hii au dawa nyengine yoyote ya kulevya ya nakotiki au saikotropiki iliyoainishwa na Waziri kwa tangazo lililochapishwa katika Gazeti, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Tatu na isiyozidi Shilingi Milioni Tano au kifungo cha mwaka mmoja au adhabu zote faini na kifungo; au

(b) mbali na zile zilizoelezwa chini ya aya ya (a) ya kifungu hiki, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Moja na Laki Tano na isiyozidi Shilingi Milioni Tatu au kifungo cha mwaka mmoja au adhabu zote faini na kifungo."

(b) kufuta vifungu vidogo vya (2) na (3).

(c) kukipa nambari upya kifungu kidogo cha (4) kuwa cha (2).

Marekebisho ya kifungu cha 30.

**15.** Kifungu cha 30 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuingiza maneno "na katika mazingira yoyote kifungo kisichopungua miaka thelathini" baada ya maneno "kifungo cha maisha".

Marekebisho ya kifungu cha 37.

**16.** Kifungu cha 37 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuingiza "19" baina ya maneno "vifungu vya" na "21" katika kifungu kidogo cha (1)(d).

Kuongeza kifungu kipya cha 41A.

**17.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 41A mara baada ya kifungu cha 41 kama ifuatavyo:

"Uwezo wa kupekua.

**41A.**-(1) Bila ya kuathiri masharti ya kibali cha upekuzi yaliyomo kwenye Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Nam. 7 ya 2018, Kamishna Mkuu au afisa aliyeidhinishwa anaweza kupekua au kutoa idhini ya maandishi kwa afisa aliye chini ya usimamizi wake kupekuwa jengo kama hali itakavyokuwa, endapo ameridhika kuwa kuna sababu za msingi za kuamini kwamba katika jengo hilo kuna kitu chochote:

(a) kinachohusiana na tuhuma za kosa linalohusiana na dawa za kulevya;

(b) ambacho kwa sababu za msingi itapelekea kupatikana ushahidi wa uhalifu kwa kosa linalohusiana na dawa za kulevya; au

(c) kilikusudiwa kutumika kwa madhumuni ya kutenda uhalifu wa kosa linalohusiana na dawa za kulevya na Kamishna Mkuu au afisa aliyeidhinishwa ameridhika kwamba ucheleweshaji wowote utapelekea kuondosha, kuharibu kitu hicho au kupoteza ushahidi.

(2) Endapo idhini yoyote chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki imetolewa, afisa anayehusika, kwa haraka iwezekanavyo, atatoa taarifa kwa Hakimu juu ya utolewaji na sababu zilizopelekea kutolewa idhini hiyo na matokeo ya upekuzi wowote uliofanywa chini ya idhini hiyo."

Marekebisho ya kifungu cha 42.

**18.** Kifungu cha 42 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (2) kwa kuingiza maneno "wa jengo" baina ya maneno "upekuzi" na "atawashirikisha".

Marekebisho ya kifungu cha 43.

**19.** Kifungu cha 43 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta maneno "kama ilivyoainishwa katika Jadweli la Nne la Sheria hii" mwisho wa kifungu kidogo cha (5).

Marekebisho ya kifungu cha 46.

**20.** Kifungu cha 46 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (2) kwa kufuta aya ya (k) na kuweka badala yake aya mpya ya (k) kama ifuatavyo:

"(k) ataandika au atasababisha kuandikwa maelezo ya mtu anayetuhumiwa kumeza aina yoyote ya dawa za kulevya yanayothibitisha usahihi wa maelezo kama ilivyoainishwa katika Fomu Nam. ZDCEA 005 chini ya Jadweli la Tano la Sheria hii."

Marekebisho ya kifungu cha 48.

**21.** Kifungu cha 48 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kufuta aya ya (c) na kuweka badala yake aya mpya ya (c) kama ifuatavyo:

"(c) kutomzuia mtu kwa muda unaozidi saa arobaini na nane isipokuwa ombi la kuongeza muda limefanywa katika Mahakama na kukubaliwa."

(b) kufuta aya ya (g) na kuweka badala yake aya mpya ya (g) kama ifuatavyo:

"(g) atachukua maelezo na kutoa risiti ya kutunza mali iliyokamatwa ya mtuhumiwa akiwa mahabusu."

Marekebisho ya kifungu cha 50.

**22.** Kifungu cha 50 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (1) kwa kufuta aya ya (d).

Marekebisho ya kifungu cha 61.

**23.** Kifungu cha 61 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (1) kwa kufuta aya ya (b) na kuweka badala yake aya mpya ya (b) kama ifuatavyo:

"(b) anamwachia au anasababisha mtu ambaye amekamatwa, anatuhumiwa, anashikiliwa au yupo chini ya uangalizi wa Mamlaka kutoroka."

Kufuta na kuweka badala yake kifungu kipya cha 72.

**24.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kufuta kifungu cha 72 na kuweka badala yake kifungu kipya cha 72 kama ifuatavyo:

"Kusitishwa kwa akaunti ya benki.

**72.**-(1) Kamishna Mkuu, katika kutekeleza kazi chini ya Sheria hii, atakuwa na uwezo wa kusitisha kwa muda matumizi ya akaunti ya benki yoyote kupisha uchunguzi wa kosa lolote chini ya Sheria hii.

(2) Mtu ambaye anakiuka au anashindwa kufuata amri ya kusitisha akaunti chini ya kifungu hiki, ametenda kosa."

Kuongeza kifungu kipya cha 76A.

**25.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 76A mara baada ya kifungu cha 76 kama ifuatavyo:

"Matumizi ya Sheria ya Utakatishaji wa Fedha Haramu na Mapato Yatokanayo na Uhalifu, Nam. 10 ya 2009.

**76A.** Bila ya kujali masharti chini ya Sheria hii, masharti ya Sehemu ya Nne, Tano na Sita ya Sheria ya Utakatishaji wa Fedha Haramu na Mapato Yatokanayo na Uhalifu, Nam. 10 ya 2009 yanaweza kutumika pamoja na mabadiliko muhimu kuhusiana na utaifishaji chini ya Sheria hii."

Marekebisho ya Jadweli la Tano.

**26.** Jadweli la Tano la Sheria Mama linarekebishwa kwa kufuta kichwa cha habari "CHETI KINACHOTHIBITISHA USAHIHI WA MAELEZO" na kuweka badala yake kichwa cha habari kipya "MAELEZO YA MTUHUMIWA ALIYEMEZA DAWA ZA KULEVYA."

## SEHEMU YA NNE
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA SHIRIKA LA MAWASILIANO ZANZIBAR, NAM. 4 YA 2023

Kusomwa.

**27.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Shirika la Mawasiliano Zanzibar, Nam. 4 ya 2023 ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 3.

**28.** Kifungu cha 3 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika ufafanuzi wa **neno** "Miundombinu ya Kimkakati ya TEHAMA" kwa kuongeza maneno "Taifa cha" kabla ya neno "kuhifadhia".

## SEHEMU YA TANO
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO, NAM. 1 YA 2003

Kusomwa.

**29.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo, Nam. 1 ya 2003 ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 4.

**30.** Kifungu cha 4 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (1) kwa:

(a) kuingiza aya mpya za (k), (l), (m) na (n) mara baada ya aya ya (j) kama ifuatavyo:

"(k) kufanya shughuli za kiuchumi, biashara na uwekezaji kwa mujibu wa sheria;

(l) kufanya ukaguzi wa vyombo vya usafiri bandarini na baharini endapo kuna taarifa zinazoshukiwa kuhusiana na magendo;

(m) kutoa msaada kwa taasisi yoyote kuhusiana na kazi za KMKM; na

(n) kutoa mafunzo kwa jamii kuhusiana na kazi zinazotekelezwa na KMKM."

(b) kuibadilisha aya ya (k) kuwa aya ya (o).

## SEHEMU YA SITA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA KIKOSI CHA VALANTIA, NAM. 5 YA 2004

Kusomwa.

**31.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Kikosi cha Valantia, Nam. 5 ya 2004 ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 4.

**32.** Kifungu cha 4 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kuingiza aya mpya ya (e) kama ifuatavyo:

"(e) kufanya shughuli ya kiuchumi, biashara na uwekezaji kwa mujibu wa sheria;"

(b) kuzibadilisha aya za (e) na (f) kuwa aya za (f) na (g).

Marekebisho ya kifungu cha 25.

**33.** Kifungu cha 25 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika aya ya (e) kwa kufuta maneno "ishirini na moja" baina ya maneno "zaidi ya" na "siku" na kuweka badala yake neno "thelathini".

## SEHEMU YA SABA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA WAKALA WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI ZANZIBAR, NAM. 2 YA 2022

Kusomwa.

**34.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar, Nam. 2 ya 2022 ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 2.

**35.** Kifungu cha 2 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuingiza maneno mapya ya ufafanuzi katika mpangilio wake wa kialfabeti kama ifuatavyo:

"mradi" maana yake ni mradi ulioanzishwa au unaoendeshwa na kikundi cha watu, mtu binafsi au taasisi ambayo inafanya biashara au inazalisha bidhaa au inatoa huduma kwa ajili ya kupata faida;

"mradi wa kati" maana yake ni mradi wowote wenye jumla ya rasilimali zenye thamani isiyopungua Shilingi Milioni Hamsini na Saba na isiozidi Shilingi Milioni Mia Sita na Hamsini au una wafanyakazi wasiopungua ishirini na wasiozidi tisini na tisa;

"mradi mdogomdogo" maana yake ni mradi wowote wenye jumla ya rasilimali zenye thamani isiozidi Shilingi Milioni Kumi na Moja au una wafanyakazi wasiozidi wanne;

"mradi mdogo" maana yake ni mradi wowote wenye jumla ya rasilimali zenye thamani inayozidi Shilingi Milioni Kumi na Moja na isiyozidi Shilingi Milioni Hamsini na Saba au una wafanyakazi wasiopungua watano na wasiozidi kumi na tisa;

Marekebisho ya kifungu cha 6.

**36.** Kifungu cha 6 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kuingiza aya mpya za (t), (u), (v) na (w) mara baada ya aya ya (s) kama ifuatavyo:

"(t) kuimarisha uwezo kwa kuwapatia wahusika wa miradi hiyo misaada ya kiufundi wa kushindana wa bidhaa za miradi Midogo midogo, Midogo na ya Kati;

(u) kuwezesha miradi Midogo midogo, Midogo na ya Kati kupata vifaa muafaka vya kufanyia kazi zao ama kwa njia ya kununua, kukodi au kwa makubaliano ya kibiashara;

(v) kuratibu, kuoanisha na kuwezesha shughuli, miradi na mipango ya pamoja ya maendeleo ya taasisi mbalimbali za umma na za binafsi kuhusiana na miradi Midogo midogo, Midogo na ya Kati;

(w) kupendekeza kwa Waziri vivutio vitakavyoshajihisha uanzishwaji na uwezeshaji wa mazingira ya kuilinda miradi Midogo midogo, Midogo na ya Kati;

(b) kuibadilisha aya ya (t) kuwa aya ya (x).

Marekebisho ya kifungu cha 42.

**37.** Kifungu cha 42 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta vifungu vidogo vya (2) na (3) na kuweka badala yake vifungu vidogo vipya vya (2) na (3) kama ifuatavyo:

"(2) Sheria ya Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati, Nam. 2 ya 2018 inafutwa.

(3) Bila ya kujali masharti chini ya vifungu vidogo vya (1) na (2) vya kifungu hiki, jambo lolote lililofanywa au kukusudiwa kufanywa chini ya Tangazo la Kisheria Nam. 114 la 2015 na Sheria ya Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati, Nam. 2 ya 2018 kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii litaendelea kuwa halali na kuchukuliwa kuwa limefanywa chini ya masharti ya Sheria hii."

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 24 Juni, 2024.

..............................................

(RAYA ISSA MSELLEM)

***Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.***